EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH
IN TANZANIA - IRINGA DIOCESE
BOMALANG'OMBE SECONDARY SCHOOL

KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI
TANZANIA - DAYOSISI YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI BOMALANG'OMBE


**Bomalang'ombe Secondary School**
P.O.BOX 1538 – **IRINGA**
Email: headmaster@bss.ac.tz or info@bss.ac.tz
Website: www.bss.ac.tz
Facebook: Bomalang'ombe secondary school
MOBILE: 0714420979/ 0768800170/ 0769343959

Our motto **"THE IMPOSSIBLE IS POSSIBLE"- MATHEW 19:26**

JINA LA MWANAFUNZI: ____________________________________________

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA BOMALANG'OMBE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026**

## 1.0. UTANGULIZI:

Uongozi wa shule pamoja na wanafunzi wote tunakupongeza kwa kuchaguliwa kwako na kujiunga na shule hii. Shule yetu inamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Iringa na imesajiliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa namba S.1831. Shule iko katika Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Kilolo, Tarafa ya Kilolo, Kata ya Bomalang'ombe. Shule ipo umbali wa Km.76 kutoka stendi kuu ya mabasi kuelekea Kusini mashariki mwa Mkoa wa Iringa na km 55 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Kilolo. Hali ya hewa ni baridi na joto kiasi hivyo sweta na blanketi ni muhimu.

Shule hii huendeshwa kwa kutegemea fedha inayolipwa na wanafunzi kwa njia ya ada. Hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kulipa ada kabla ya kupewa huduma za kitaaluma, chakula na malazi. Ni matumaini yetu kuwa utaitumia nafasi hii ipasavyo kwa manufaa yako binafsi, wazazi, kanisa na Taifa letu kwa ujumla. "KARIBU SANA BOMALANG'OMBE SEKONDARI".

## 1.1. MKAZO WA SHULE:

Shule hukazia sana **Maadili Mema** na **Taaluma (visual changes)** ya wanafunzi. Hivyo huendeshwa kwa kuzingatia misingi ya kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania- Dayosisi ya Iringa. Madhehebu mengine yanakaribishwa kuishi pamoja nasi. **LAKINI** sio kuja kutufundisha itikadi zao. Mwanafunzi akiona hawezi kuendana nasi basi tunashauri atafute shule nyingine itakayoendana na matakwa yake.

**ADA YA SHULE**

Ada ya shule kwa mwaka kuanzia kidato cha **I - VI** ni shilingi **1,470,000/= tu**

**Bomalang'ombe Secondary School**
P.O.BOX 1538 – **IRINGA**
Email: headmaster@bss.ac.tz or info@bss.ac.tz
Website: www.bss.ac.tz
Facebook: Bomalang'ombe secondary school
MOBILE: 0714420979/ 0768800170/ 0769343959
Our motto **"THE IMPOSSIBLE IS POSSIBLE"- MATHEW 19:26**

**MZAZI/MLEZI WA**____________________________________________________

## MCHANGANUO WA JINSI YA ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA I - VI MWAKA 2026

### A. ADA YA MWAKA

| | JANUARI AWAMU 1 | APRILI AWAMU 2 | JULAI AWAMU 3 | SEPTEMBA AWAMU 4 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| **KIDATO CHA I – VI** | 400,000/= | 335,000/= | 400,000/= | 335,000/= | **1,470,000/=** |

### B. ADA YA MITIHANI KWA KIDATO CHA II_& VI

| KIDATO | MTIHANI | ADA YA MTIHANI |
|---|---|---|
| **KIDATO CHA II** | Mtihani wa taifa | 15,000/= |
| | Mock DIRA | 20,000/= |
| | Mock mkoa | 20,000/= |
| | CSSC | 20,000/= |
| | **JUMLA** | **75,000/=** |
| **KIDATO CHA IV** | Mtihani wa taifa | 50,000/= |
| | Mock DIRA | 20,000/= |
| | Mock Mkoa | 20,000/= |
| | CSSC | 20,000/= |
| | **JUMLA** | **110,000/=** |

**Fedha ya mtihani kwa kidato cha pili, cha nne na cha sita ipo nje ya malipo ya ada ya mwaka. Ilipwe mapema Januari.**

Malipo yote yafanyike kupitia benki kwa akaunti zifuatazo:

i) Absa Benki **A/C 0536001417** Bomalang'ombe sekondari.
ii) CRDB Benki **A/C 0150243260300** Bomalang'ombe sekondari

**Ifahamike kuwa mzazi atakayeleta fedha taslimu hatutapokea. Mwanafunzi aje na stakabadhi halisi ya malipo ya benki (BANK PAY IN SLIP)**

Iwapo unahitaji ufafanuzi wowote unaohusu malipo ya ada,

**Wasiliana na :**

a) Mkuu wa shule............................................ **0714420979/0768800170**
b) **Makamu Mkuu wa Shule** ………………….. **0687899071/0769343959**
c) Mhasibu wa shule………………………………. **0745411241**

.............................................

**TIBERRY MBOSSA**
**MKUU WA SHULE**

**MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

3.1. **Sare za shule**

- Mashati (2) meupe (mikono mirefu), soksi (kwa wasichana ndefu mpaka magotini) (2) nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi jozi(2), raba za michezo, nguo za michezo aje navyo,
- Track suit rangi nyeusi yenye miraba myeupe na jaketi zito jeusi kwa ajili ya kuvaa wakati wa baridi sana.
- Sare zingine zote zinapatikana shuleni kwa gharama zilizooneshwa hapa chini.
  - Sketi (4) Tshs 80,000/= (2) za kushindia nje na (2) za darasani
  - Suruali (4) Tshs 80,000/= (2) za kushindia nje na (2) za darasani
  - Sweta bluu (1) Tshs. 15,000/=
  - T.shirt (1) rangi ya njano (sare) kwa Tsh. 15,000/=
  - T.shirt (2) za kazi (nevi bluu ) kwa Tsh. 30,000/=

    **Zote zitapatikana hapa hapa shuleni.**

**Malipo yote ya sare za shule yafanyike kupitia Absa A/C 0536001417 - Bomalang'ombe sekondari.**

3.2. VIFAA VYA TAALUMA

Wanafunzi wote wanatakiwa waje na daftari za kutosha (11), box file 1, kalamu, rula, seti ya hesabu, rimu ya karatasi A4 mbili (2) (**Januari 1, Julai 1**), anunuliwe vitabu vya kiada (Text books) walau vya masomo 3, vitabu hivi viwe ni vya kidato husika. Biblia (Holy Bible) ni ya LAZIMA kwa wakristo wote na kitabu cha nyimbo kwa Walutheri ni LAZIMA.

3.3. <u>MAHITAJI MENGINE</u>

Mashuka (2) ya pinki, blanket (1), mto (1), foronya (pink), sanduku la bati dogo, vifaa vya chakula, jembe na mpini, ndoo ya lita 10 ya bluu,Mfagio1(Chelewa) na Tshs 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho.

**NB: Shule inatoa huduma ya Godoro hivyo mwanafunzi asije na godoro shuleni**

3.4. Shule haina huduma ya chakula maalumu (special diet)

***NB: Kila mwanafunzi atalazimika kushiriki katika miradi ya shule kama vile kulima bustani za shule na kushiriki katika ufugaji ikiwa ni sehemu ya kujitegemea "Self-reliance".***

## 4.0. TAALUMA:

4.1. Ni matarajio yetu kuwa kila mwanafunzi atafanya bidii kujifunza na kufaulu kwa viwango vya A, B, au C. Hii inawezekana tu kwa mwanafunzi anayejituma, anayemhurumia anayemlipia ada na mwenye malengo ya ushindani kitaaluma.

## 5.0. MGAWANYO WA MAJUKUMU:

### 5.1. Mzazi/Mlezi/Mfadhili

Ni wajibu wake kulipa ada kikamilifu, kufuatilia maendeleo ya mwanae na kujenga ushirikiano na mwalimu.

### 5.2. Mwanafunzi

Atawajibika kusoma kwa bidii na maarifa, kuuliza walimu asipoelewa na kuhakikisha anapata alama A, B au C tu.

**5.3. Walimu**

Kumfundisha mwanafunzi mpaka anapoelewa vema, kumlea kitaaluma, kiroho, kiakili, kimwili, kiuchumi na kisiasa. Kumtumia mzazi ripoti ya maendeleo ya mwanafunzi.

**TAARIFA ZINGINE**

**6.1. Uthibitisho wa daktari**

Kila mwanafunzi **LAZIMA** apime afya yake kabla ya kuja shuleni. Fomu ya kupimia imeambatanishwa na fomu hii. Kwa watoto wenye matatizo sugu tunashauri wasome shule jirani na Hospitali kubwa.

**6.2.** Shule itafunguliwa tarehe **05/01/ 2026.**

**USAFIRI**

Kuna mabasi mawili na costa moja yanayofanya safari kati ya Iringa na Bomalang'ombe

**7.1 Nauli:** Iringa – Bomlang'ombe Tshs. **8,000/=**

**NB:** Tumia mabasi ya **Mwafrika**, **Upendo na costa ya Mponda ,** usafiri huu unapatikana katika stendi ya mabasi ya Mlandege, utakufikisha mpaka Bomalang'ombe.

**7.2 KUTOFIKA SHULENI**

Tafadhali kama umeahirisha kujiunga na shule yetu kwa sababu yoyote ile, tunaomba tutaarifiwe kwa namba za simu zilizopo katika ukurasa wa kwanza wa fomu hii. Hii itatusaidia kutoa nafasi kwa wanafunzi waliokosa nafasi.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA SAFARI NJEMA YA KUJA SHULENI KWAKO**

**BOMALANG'OMBE SEKONDARI.**

**KARIBU SANA**

**TIBERRY MBOSSA**

**MKUU WA SHULE**

# SHERIA/KANUNI ZA SHULE JUU YA NIDHAMU YA WANAFUNZI

Shule ya Sekondari Bomalang'ombe ni mali ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania – Dayosisi ya Iringa na inaendeshwa kwa kuzingatia miongozo, taratibu, kanuni na sheria za maadili ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania – Dayosisi ya Iringa na zile za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

## 1.0. MATARAJIO:

Ni matarajio yetu kuwa kila mwanafunzi atazingatia yafuatayo:-

1.1. Ataheshimu ratiba yote ya shule.
1.2. Ataheshimu watumishi wote wa shule, majirani, wanafunzi wenzake na kila atakayekutana naye
1.3. Atavaa mavazi ya heshima.
1.4. Atazingatia kwa makini suala la taaluma ambalo ndilo msingi hapa shuleni.
1.5. Hatakuwa kikwazo kwa wenzake na kuwa mfano mbaya kwa Kanisa na Taifa kwa ujumla.
1.6. Mwanafunzi atatunza fedha ya matumizi kwa Mhasibu wa shule. Shule haitahusika na upotevu wa fedha zilizotunzwa bwenini.
1.7. Kila Mwanafunzi atarudi nyumbani baada ya kupata ruhusa ya maandishi na atamwonyesha mzazi/mlezi wake. Vingivevyo atahesabika kuwa mtoro.

## 2.0. KUTO MILIKI SIMU SHULENI

Mwanafunzi yeyote yule haruhusiwi kumiliki simu hapa shuleni. Pia ifahamike kuwa mwanao akikupigia simu bila kupitia kwa Mkuu wa shule, ofisi ya malezi au taaluma au mtumishi yoyote aliyeteuliwa, anafanya kosa kubwa. Taarifa zake zihesabike kuwa ni **utovu wa nidhamu, k**ama sio **uzushi**. Mtoto mwenye **kunena** na **kutenda** haki ni jasiri wa kuwaelezea matatizo yake walezi wake hapa shuleni **(Mithali 28:1)**

## 3.0. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

1. Wizi wa aina yoyote ile
2. Uasherati, ubakaji na ushoga shuleni na nyumbani.
3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa sigara au bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kupata au kusababisha Mimba ndani na nje ya shule
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutoa mimba
10. Utoro wa aina yoyote ile
11. Kutohudhuria vipindi darasani na kutofanya mazoezi.
12. Kugoma, kuchochea, kushawishi na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kutolipa ada ya shule na dahalia.
15. Kulala nje ya bweni alilopangiwa
16. Kutofanya vizuri katika taaluma hasa kujipatia wastani wa F, E au D katika mitihani.
17. Kutohudhuria ibada mbalimbali
18. Tabia ya kuchelewa kufungua shule katika tarehe iliyopangwa.
19. Kuvaa mlegezo au sketi fupi (juu ya magoti).
20. Kusema au kutetea uongo.

**Bomalang'ombe Secondary School**
P.O.BOX 1538 – **IRINGA**
Email: headmaster@bss.ac.tz or info@bss.ac.tz
Website: www.bss.ac.tz
Facebook: Bomalang'ombe secondary school
MOBILE: 0714420979/ 0768800170/ 0769211663
Our motto **"THE IMPOSSIBLE IS POSSIBLE"- MATHEW 19:26**


---

TO THE MEDICAL OFFICER,

…………………………………….

…………………………………….

**RE**: ……………………………………………………………………………………………….

Please examine the above named person as to his/her fitness to first studies in the school.

Eye………………………………………………………………………………………….

Ears …………………………………………………………………………………………

Chest………………………………………………………………………………………..

Spleen……………………………………………………………………………………….

Stool…………………………………………………………………………………………

Urine ………………………………………………………………………………………..

Blood ……………………………………………………………………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examine the above named person, and considered that

…………………………………………...…………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………..…………………………………………………………

Date……………………………………………………..

Signature………………………………..

Hospital/Health Centre………………………………

Designation……………………………..

**EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA - IRINGA DIOCESE**

**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA - DAYOSISI YA IRINGA**

**BOMALANG'OMBE SECONDARY SCHOOL**

**SHULE YA SEKONDARI BOMALANG'OMBE**

E. L. C. T - IRINGA DIOCESE
BOMA LA NG'OMBE SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 1538
IRINGA
The Impossible Is Possible

**Bomalang'ombe Secondary School**
P.O.BOX 1538 – **IRINGA**
Email: headmaster@bss.ac.tz or info@bss.ac.tz
Website: www.bss.ac.tz
Facebook: Bomalang'ombe secondary school
MOBILE: 0714420979/ 0768800170/ 0769343959
Our motto **"THE IMPOSSIBLE IS POSSIBLE"- MATHEW 19:26**

E. L. C. T - IRINGA DIOCESE
BOMA LA NG'OMBE SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 1538
IRINGA
The Impossible Is Possible

TAREHE …………………………………..

MZAZI.MLEZI WA …………………………………………………………………………………..

## MAKUBALIANO YA KITAALUMA, NIDHAMU NA ULIPAJI WA ADA

### A. TAAALUMA NA NIDHAMU

Mimi …………………………………… Mzazi/mlezi/Mfadhili wa ……………………. ……………………………………………(Mwanafunzi) kidato cha …………………….. Nimesoma masharti na maelekezo ya kujiunga na shule hii na kuyaelewa vizuri. Baada ya kusoma nimekubaliana nayo na niko tayari kufuata utaratibu huu maana ninaamini utaleta ushindani mzuri wa kitaaluma. Kwa upande wa sheria na kanuni za shule, juu ya nidhamu ya wanafunzi,tunakiri/ninakiri wazi kuwa tumesoma/nimesoma na kuelewa (mzazi/mlezi na mtoto ) kuwa shule ina nia nzuri katika kulea wanafunzi wetu.

### B. ULIPAJI WA ADA

Nitakuwa tayari kulipa ada kwa mtindo uliopendekezwa hapo juu.

**Muhimu:** Unaweza kulipa ada kwa awamu moja, mbili au tatu kulingana na uwezo wako.

Mwisho wa malipo yote ni mwezi wa tisa (9).

Anuani ya Mzazi/Mlezi ya sasa …………………………………………………………
Namba ya simu ya mzazi/mlezi ……………………………………………………….
Jina la Mzazi/Mlezi/Mfadhili ………………………………………………………….
Sahihi ya Mzazi/Mlezi/Mfadhili ………………….Sahihi ya mwanafunzi …………….

**NB.** Fomu hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule. Pia, ieleweke kuwa mwanafunzi hatapokelewa shuleni bila fomu hii kwa sababu yoyote ile.

Mzazi/Mlezi/Mfadhili lipa ada kikamilifu kwa maendeleo ya mwanao, shule, kanisa na Taifa kwa ujumla.

…………………………..
**TIBERRY MBOSSA**

**MKUU WA SHULE**